BENKI KUU YA TANZANIA



# Tathmini Ya Mwenendo Wa Uchumi

Desemba 2025

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia........1

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa........3

2.1 Mfumuko wa Bei........3

2.2 Sera ya Fedha........5

2.3 Viwango vya Riba........6

2.4 Masoko ya Fedh........7

2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali........8

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa........9

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje........11

3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar........13

3.1 Mfumuko wa Bei........13

3.2 Shughuli za Bajeti ya Serikali........14

3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje........14

Viambatisho........17

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia katika kipindi cha mwaka 2025 ulikabiliwa na misukosuko iliyotokana na kuongezeka kwa mivutano ya kibiashara, migogoro ya kisiasa na kutotabirika kwa sera za kimataifa. Pamoja na changamoto hizo, kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi ilionesha uthabiti kuliko ilivyotarajiwa.

Maoteo ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Shirika la ushirikiano wa Kiuchumi na Manendeleo(OECD) yanaonesha kuimarika kwa ukuaji, kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mwaka 2024[1], ikichangiwa na utekelezaji wa sera za fedha za kubana na migogoro ya kibiashara. Uwekezaji, hususan katika nchi zinazoibukia kiuchumi, unatarajiwa kuwa kichocheo kikuu cha matokeo hayo. Katika robo ya nne ya mwaka 2025, nchi zilizoendelea kiuchumi zinatarajiwa kuwa na uchumi imara zaidi, ukichangiwa na kuimarika kwa matumizi ya watu na uwekezaji. Ingawa fahirisi za kutokuwa na uhakika wa sera za kibiashara duniani imepungua kutoka viwango vya juu vilivyorekodiwa mwezi Septemba 2025, viwango hivyo bado ni vya juu kwa kulinganisha na mwenendo wa kihistoria, hali inayopelekea makampuni kuendelea kutekeleza mikakati ya tahadhari katika kufanya maamuzi ya uwekezaji wa mitaji na urekebishaji wa kinga za minyororo ya ugavi ya kimataifa (Kielelezo 1.1 a and 1.1b). Mtazamo wa muda wa kati unaonesha kuendelea kuwepo kwa vihatarishi kutokana na utekelezaji wa sera za kujihami na mazingira yanayoendelea kubadilika ya vikwazo vya biashara za kimataifa.

[1] Tathmini ya Uchumi wa Dunia (World Economic Outlook) ya Oktoba 2025, IMF ilipandisha makadirio yake ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 hadi asilimia 3.2, kutoka asilimia 3.0 yaliyotolewa Julai 2025, sambamba na tathmini iliyotolewa na OECD mwezi Septemba 2025, ambayo pia ilipandisha maoteo ya ukuaji mwaka 2025 hadi asilimia 3.2, kutoka asilimia 2.9 mwezi Juni 2025.

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Kwa muktadha huu, mwenendo katika masoko ya bidhaa umeakisi hali ya kupungua kwa mahitaji katika masoko ya kimatifa, mabadiliko katika mtazamo wa hatari, na mwenendo unaobadilika wa hali ya ugavi (Kielelezo 1.2). Katika masoko ya nishati, bei za mafuta ghafi ziliendelea kushuka mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na mwezi uliotangulia, hali iliyochochewa na ongezeko la uzalishaji kutoka kwa nchi za OPEC+ na zisizo za OPEC+, pamoja na kuendelea kupungua kwa mahitaji duniani. Wakati huo huo, bei za dhahabu zilipanda kwa rekodi ya juu, zikichangiwa na ongezeko la mahitaji kama hifadhi salama na matarajio ya kupungua zaidi kwa viwango vya riba katika nchi zilizoendelea, jambo linalopunguza gharama ya fursa ya kushikilia dhahabu[2].

[2] Banki ya Marekani (Federal Reserve) ilipunguza kiwango cha riba kwa pointi 25 mwanzoni mwa Disemba 2025, na kupunguza wigo wa lengo hadi asilimia 3.50 – 3.75

Mwenendo wa bei za bidhaa za kilimo ulikuwa mchanganyiko. Bei za kahawa aina ya Arabika ziliongezeka kwa kiwango cha wastani, ingawa ongezeko hilo lilipunguzwa na mwelekeo wa kuongezeka kwa uhitaji wa kahawa aina ya Robusta, ambayo bei yake iliendelea kuwa tulivu kutokana na kuimarika kwa uzalishaji nchini Brazil na Vietnam. Bei za mafuta ya mawese zilishuka kutokana na uzalishaji mkubwa nchini Malaysia na Indonesia.

Bei za mahindi ziliendelea kuwa juu, kutokana na uhitaji mkubwa pamoja na taarifa za hali mbaya ya hewa nchini Brazil na Argentina, nchi ambazo ni wazalishajii wakubwa wa mahindi duniani. Bei za ngano ziliongezeka, kutokana na matarajio ya mahitaji zaidi kutoka Uchina, mvutano wa siasa za kimataifa katika eneo la Bahari Nyeusi, na matarajio ya kushuka kwa uzalishaji nchini Urusi.Aidha, bei za sukari zilishuka, kutokana na ongezeko la uzalishaji nchini Brazil, India na Thailand, pamoja na kupungua kwa matumizi ya sukari katika uzalishaji wa *ethanol* kufuatia kushuka kwa bei za mafuta ghafi.

**Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia**




Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi mbalimbali. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei ulirekodiwa kupungua, kwa kasi tofauti katika nchi mbalimbali, hali iliyochangiwa na kushuka kwa bei za nishati na kuimarika kwa hali ya ugavi (Kielelezo 1.3). Nchini Uingereza na katika soko la pamoja la Ulaya, mfumuko wa bei ulibakia karibu na kiwango cha lengo la sera ya fedha.

Kwa ujumla, mfumko wa bei ulikuwa na mwenendo wa kupungua katika nchi zinazoibukia kiuchumi, ingawa kasi ya kupungua iliathiriwa kwa utofauti katika kila nchi. Nchini Uchina, mfumuko wa bei uliongezeka kidogo, ukichochewa na gharama za chakula. Nchini India, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na kupungua kwa bei za chakula pamoja na kuchelewa kwa athari za hatua za awali za kubana kwa sera za fedha[3].

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

Katika kanda za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), mfumuko wa bei umekuwa na muelekeo wa kushuka kuelekea kwenye viwango vya ulinganifu wa mtangamano wa kikanda (Kielelezo 1.4 na 1.5).Matokeo haya yalichangiwa na kushuka kwa gharama za chakula na mafuta pamoja na utekelezaji wa sera za kiuchumi.

Kwa kuzingatia hali hiyo, benki kuu kwa uangalifu zilipunguza viwango vya riba pale tu mfumuko wa bei ulipoonekana kupungua zaidi, na kuongeza viwango vya riba katika mazingira ya mfumuko wa bei au hali ya kutotabirika. Nchi zinazoibukia ziliweka uwiano wa kupungua kwa mfumko wa bei kulingana na hali ya viwango vya kubadilisha fedha na akiba ya fedha ya kigeni kwa umakini ili kukabiliana na vihatarishi vya nje.

[3] IMF 2025, na OECD, 2025.

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu

Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**




Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu

Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei ulikuwa wa chini na tulivu katika kiwango cha asilimia 3.4 mwezi Novemba 2025, kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na kupungua kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, hususan mafuta (Kielelezo 2.1.1 na Jedwali 2.1.1).

Mfumuko wa bei ulibaki ndani ya wigo wa malengo ya kitaifa wa asilimia 3–5, sambamba na vigezo vya mtangamano vya SADC na EAC (Kielelezo 2.1.3). Mfumuko wa bei ya mazao ya vyakula vikuu na mazao ya vyakula mbadala uliendelea kuwa tulivu licha ya ongezeko la bei za bidhaa muhimu za chakula, hususan mchele na ngano (Kielelezo 2.1.2a na 2.1.2b).

**Kielelezo 2.1.1: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili.**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Jedwali 2.1.1: Maendeleo ya Mfumuko wa Bei**

2020 = 100

| | | Badiriko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiriko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiriko kwa Mwaka | | |
| Mfumuko wa bei katika Makundi Makuu | Mizania | Nov-24 | Okt-25 | Nov-25 | Nov-24 | Okt-25 | Nov-25 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 1.2 | -0.2 | 0.4 | 3.3 | 7.4 | 6.6 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 1.8 | 3.6 | 3.5 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 1.6 | 2.0 | 2.0 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | 0.1 | -0.5 | -0.2 | 4.1 | 2.4 | 2.2 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa | 7.9 | 0.3 | 0.3 | 0.2 | 2.1 | 3.1 | 3.0 |
| Afya | 2.5 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 1.8 | 1.2 | 1.3 |
| Usafiri | 14.1 | 0.1 | -0.7 | 1.3 | 3.8 | 1.7 | 2.9 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.1 | 0.1 | 0.0 | 1.2 | 0.3 | 0.3 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 0.3 | 0.0 | -0.2 | 2.0 | 1.0 | 0.4 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 3.1 | 3.0 | 3.0 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 2.6 | 1.0 | 1.0 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.0 | -0.1 | 1.2 | 0.4 | 0.3 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.1 | -0.2 | 0.3 | 6.3 | 1.6 | 1.7 |
| Mfumuko wa bei kwa Bidhaa Zote | 100.0 | 0.4 | -0.2 | 0.3 | 3.0 | 3.5 | 3.4 |
| Mfumuko wa bei katika Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Bidhaa za Msingi | 73.9 | 0.3 | -0.1 | 0.5 | 3.3 | 2.1 | 2.3 |
| Mfumuko usiojumuisha mfumko wa Bidhaa za Msingi | 26.1 | 0.9 | -0.4 | -0.1 | 2.1 | 7.3 | 6.2 |
| Mfumuko wa bei za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | -0.2 | -1.4 | -0.5 | 5.7 | 4.0 | 3.8 |
| Mfumuko wa bei za Huduma | 37.2 | 0.1 | -0.3 | 0.6 | 2.3 | 1.0 | 1.6 |
| Mfumuko wa bei za Bidhaa | 62.8 | 0.7 | -0.1 | 0.2 | 3.3 | 5.0 | 4.4 |
| Mfumuko wa bei za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 0.2 | -0.2 | 0.1 | 3.1 | 2.6 | 2.4 |
| Mfumuko wa bei za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 0.1 | -0.2 | 0.3 | 2.9 | 1.9 | 2.1 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Kielelezo 2.1.2: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao**

**a. Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu

**b. Mazao Vyakula Mbadala**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.3: Mfumuko wa Bei na Malengo Yake**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Akiba ya mahindi iliyopo katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ilipungua hadi tani 590,424.7, baada ya utoaji wa mahindi kwa wafanyabiashara na Mpango wa Chakula Duniani (tani 11,667.4) kuzidi ununuzi mpya (tani 8,607.6) (Jedwali 2.1.2). Uuzaji huo ulisaidia kupunguza shinikizo la kupanda kwa bei za chakula.

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 43,597 | 110,398 | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 |
| Feb | 41,231 | 110,389 | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 |
| Mac | 39,597 | 109,231 | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 |
| Apr | 38,053 | 109,231 | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 |
| Mei | 38,291 | 108,284 | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 |
| Jun | 52,725 | 107,384 | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 |
| Jul | 90,255 | 107,384 | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 |
| Ago | 92,991 | 123,635 | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 |
| Sep | 109,733 | 150,057 | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 |
| Okt | 110,895 | 192,408 | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 |
| Nov | 110,289 | 209,057 | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 |
| Des | 110,398 | 214,968 | 137,655 | 248,282 | 677,115 | |

Chanzo:Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula

Mfumuko wa bei wa msingi ulipungua hadi asilimia 2.3 mwezi Novemba 2025 kutoka asilimia 3.3 iliyorekodiwa katika mwezi kama huo mwaka uliopita, ikichangiwa na kushuka kwa bei za baadhi ya bidhaa, zikiwemo nguo, sare za shule, magari yaliyotumika, pamoja na bidhaa zilizofungashwa kama mafuta ya alizeti na maji ya chupa (Jedwali 2.1.1).

Mfumuko wa bei za mafuta, nishati na bili za maji zilipungua hadi asilimia 3.8 kutoka asilimia 5.7 mwezi Novemba 2024, ikiakisi kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Bei za petroli nchini zilishuka kutoka kilele cha shilingi 3,435.3 katikati ya mwaka hadi shilingi 2,883.1 kwa lita mwezi Novemba 2025; vilevile bei za dizeli zilishuka kutoka shilingi 3,034.8 hadi shilingi 2,834.2 kwa lita, huku wastani wa bei ya mafuta ya taa ikiendelea kuwa tulivu kwa kiwango cha shilingi 3,200 (Kielelezo 2.1.5).

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## 2.2 Sera ya Fedha

Katika kikao chake cha 239 kilichofanyika mwezi Oktoba 2025, Kamati ya Sera ya Fedha iliamua riba ya Benki Kuu (CBR) kuendelea kuwa asilimia 5.75 kwa robo ya nne ya mwaka 2025. Uamuzi huu ulifanyika kwa lengo la kuendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa kuwa mfumuko unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 3-5. Hivyo, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/-2 sambamba na CBR.

Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwezi Novemba 2025 ulikuwa wa kuridhisha, hali iliopelekea uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi katika sekta ya kibenki huku riba ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki ikiendelea kubaki ndani ya wigo (Kielelezo 2.2.1). Kufuatia kuimarika kwa hali ya ukwasi, mahitaji ya mikopo ya muda mfupi kwa mabenki kutoka Benki Kuu yalipungua, ambapo mwezi Novemba 2025 Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 645.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 869.2 zilizotolewa mwezi uliopita (Kielelezo 2.2.2). Wastani wa riba ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) ilikuwa asilimia 6.15, ndani ya wigo wa CBR.

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*extended broad money supply, M3*) ulikua kwa asilimia 23.5 mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 21.4 kwa mwezi uliotangulia na asilimia 13.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Ukuaji huu ulichagizwa zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi ambayo ilikua kwa asilimia 18.1, ikilinganishwa na asilimia 16.1 kwa mwezi uliopita na asilimia 15.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.2.4 na 2.2.5).

Wakati huohuo, mikopo ilioelekezwa kwenye shughuli za uchimbaji madini ilikua kwa asilimia 30.1, ikifuatiwa na sekta ya biashara na kilimo ziilizokuwa na ukuaji wa asilimia 29.4 na 27.0, mtawalia (Jedwali 2.2.2). Mikopo kwa shughuli binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa hutumika kugharamia biashara ndogo sana, ndogo na

za kati iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikiwa na asilimia 35.8, ikifuatiwa na shughuli za biashara kwa asilimia 13.6 na kilimo kwa asilimia 13.0 (Kielelezo 2.2.6).

### Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| | Kiasi (Shilingi Billioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipengele** | Okt-24 | Okt-25 | Nov-25 | Okt-24 | Okt-25 | Nov-25 |
| Rasilimali halisi za nje | 13,773.6 | 15,715.4 | 16,298.6 | 42.3 | 14.1 | 22.6 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 12,668.2 | 13,334.3 | 13,892.1 | 26.9 | 5.3 | 21.4 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,105.4 | 2,381.1 | 2,406.5 | --- | --- | --- |
| Rasilimali halisi za ndani | 35,469.4 | 44,073.3 | 44,586.4 | 6.6 | 24.3 | 23.1 |
| Madai rasmi ya ndani | 48,136.2 | 56,509.3 | 57,628.4 | 9.7 | 17.4 | 17.6 |
| Amana za Serikali zilizopo Ben | 7,837.1 | 8,965.9 | 9,303.8 | -12.7 | 14.4 | 16.4 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,517.8 | 42,386.9 | 43,385.6 | 17.0 | 16.1 | 18.1 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,666.9 | -12,436.1 | -13,042.0 | 19.4 | -1.8 | 2.1 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 49,243.0 | 59,788.6 | 60,885.1 | 14.6 | 21.4 | 23.0 |
| Amana za fedha za kigeni | 12,745.0 | 13,882.1 | 14,056.5 | 34.2 | 8.9 | 13.9 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 36,498.0 | 45,906.5 | 46,828.5 | 9.1 | 25.8 | 26.0 |
| Amana zinginezo | 14,224.2 | 16,848.4 | 17,618.1 | 10.3 | 18.4 | 22.7 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 22,273.8 | 29,058.1 | 29,210.4 | 8.3 | 30.5 | 28.0 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 7,408.2 | 8,410.1 | 8,571.4 | 17.3 | 13.5 | 12.8 |
| Amana za hundi | 14,865.6 | 20,648.0 | 20,639.0 | 4.3 | 38.9 | 35.6 |
| Fedha za msingi (M0) | 11,765.8 | 15,068.7 | 15,162.0 | 19.8 | 28.1 | 27.9 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.5: Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

### Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi

Asilimia

| | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 | Ago-25 | Sep-25 | Okt-25 | Nov-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | 4.0 | -36.3 | -30.6 | -28.2 | -24.8 | -10.5 | 22.9 | 20.8 | 0.8 | 3.2 | 32.4 | 29.7 | 30.1 |
| Biashara | 6.7 | 5.6 | 5.0 | 5.8 | 12.7 | 14.4 | 24.1 | 21.3 | 26.2 | 29.2 | 24.8 | 21.8 | 29.4 |
| Kilimo | 41.9 | 41.0 | 41.6 | 37.2 | 36.3 | 29.8 | 29.8 | 30.2 | 31.8 | 30.1 | 27.6 | 25.6 | 27.0 |
| Ujenzi | 16.6 | 11.6 | 19.0 | 23.1 | 35.1 | 39.2 | 27.9 | 25.7 | 21.6 | 14.8 | 15.7 | 14.2 | 22.4 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 11.3 | 13.2 | 14.8 | 14.5 | 22.4 | 23.8 | 25.6 | 25.7 | 18.9 | 18.8 | 17.4 | 18.7 | 22.1 |
| Hoteli na migahawa | -1.5 | 2.7 | 1.3 | 4.6 | 5.4 | 7.0 | 21.7 | 22.5 | 13.0 | 11.4 | 16.3 | 23.2 | 19.4 |
| Shughuli binafsi | 19.2 | 14.7 | 13.9 | 13.1 | 9.4 | 14.7 | 13.6 | 13.7 | 13.1 | 15.0 | 14.7 | 11.3 | 10.3 |
| Viwanda | 9.4 | 16.3 | 18.0 | 16.9 | 10.9 | 7.7 | 7.3 | 2.5 | 6.3 | 3.4 | 0.1 | 5.2 | 2.8 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

### Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.3 Viwango vya Riba

Riba za mikopo na amana ziliongezeka kidogo mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na mwezi uliotangulia. Wastani wa riba za mikopo uliongezeka hadi asilimia 15.27 kutoka asilimia 15.19 kwa mwezi Oktoba 2025. Wakati huohuo,riba za mikopo inayotozwa kwa wateja wakubwa (*negotiated lending rates*) zikiongezeka kidogo hadi asilimia 12.61 ikilinganishwa na asilimia 12.40 kwa mwezi uliopita (Jedwali 2.3.1).

Riba za amana ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 8.54 kutoka asilimia 8.36 mwezi Oktoba 2025, huku riba za amana kwa wateja wakubwa (*negotiated deposit rate*) zikiongezeka hadi wastani wa asilimia 11.67 kutoka asilimia 11.22 kwa mwezi uliopita. Kufuatia mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 5.51, kutoka asilimia 5.93 mwezi Novemba 2024 (Jedwali 2.3.1)

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo Inayo tolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Nov-24 | Mac-25 | Jun-25 | Sep-25 | Okt-25 | Nov-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.69 | 2.86 | 2.90 | 2.92 | 2.93 | 2.88 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.67 | 15.50 | 15.23 | 15.18 | 15.19 | 15.27 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.56 | 15.83 | 15.69 | 15.52 | 15.50 | 15.53 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.77 | 12.94 | 12.68 | 12.84 | 12.40 | 12.61 |
| Riba za amana -jumla | 8.18 | 8.00 | 8.74 | 8.50 | 8.36 | 8.54 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.63 | 8.14 | 9.79 | 9.84 | 9.21 | 10.02 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.14 | 10.35 | 11.21 | 11.05 | 11.22 | 11.67 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 5.93 | 7.69 | 5.90 | 5.69 | 6.28 | 5.51 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha

### Soko la Dhamana za Serikali

Kwa mwezi Novemba, Benki Kuu iliendesha minada miwili ya dhamana za Serikali yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 352 ambapo kiasi kikubwa kilikuwa kwa ajili ya kugharamia bajeti Serikali, huku kiwango kidogo kikiwa kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya fedha. Sanjari na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, minada hiyo ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 798.4, zaidi ya matarajio *(oversubscription)* ambapo shilingi billion 369.2 zilikubaliwa. Kufuatia mwenendo huu, riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi asilimia 6.25 ikilinganishwa na asilimia 6.27 mwezi uliotangulia(Kielelezo 2.4.1).

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki iliendesha minada ya hati fungani za miaka 5 na 15, zenye thamani ya shilingi bilioni 174.9, na shilingi bilioni 165.5, mtawalia. Hati fungani zote zilikuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyotarajiwa *(oversubscription)* hali inayoashiria kuongezeka kwa ukwasi na mahitaji ya uwekezaji kwenye hati fungani. Jumla ya zabuni zilizowasilishwa kwa minada yote miwili ilikuwa shilingi bilioni 1,008.6, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 329.3 zilikubaliwa. Wastani wa faida ulipungua kwa hati fungani ya miaka 5 hadi asilimia 10.54 na asilimia 12.08 kwa hati fungani ya miaka 15 hali inayoashiria kuimarika kwa mazingira ya ukopaji na kuendelea kuaminika kwa soko la mikopo la ndani.

## Soko la fedha baina ya mabenki

Kwa mwezi Novemba, 2025 baishara katika soko la fedha baina ya mabenki (IBCM) ilindelea kufanyika kwa ufanisi na hivyo kurahisisha usambazaji wa ukwasi wa shilingi kati ya mabenki. Sambamba na uwepo wa ukwasi wa kutosha, kiwango cha mikopo baina ya mabenki kilipungua hadi shilingi bilioni 1,781.0 kutoka shilingi bilioni 2,255.4 kwa mwezi uliotangulia huku mikopo ya siku saba ikiendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikiwa ni zaidi ya asilimia 75.7 (Kielelezo 2.4.2). Wastani wa riba katika soko ulipungua hadi asilimia 6.30 ikilinganishwa na asilimia 6.38 kwa mwezi Oktoba 2025.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha za kigeni

Katika mwezi Novemba 2025, hali ya soko la fedha za kigeni (IFEM) iliendelea kuwa tulivu, kukiwa na kiwango cha kutosha cha fedha za kigeni, hali iliochangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya nchi. Jumla ya mauzo ya fedha za kigeni katika soko yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 158.7, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 133.7 mwezi Oktoba 2025, ambapo asimilia 66.9 ya mauzo haya yalifanywa na benki za biashara. Wakati huohuo, Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa mujibu wa sera ya ushiriki katika soko la fedha za kigeni, kwa kuuza dola za Marekani milioni 52.5 (Kielelezo 2.4.3).

Sambamba na kuongezeka kwa hali ya ukwasi wa fedha za kigeni, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,444.81 kwa dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,460.54 kwa dola moja ya Marekani kwa mwezi uliopita. Hii ilikuwa sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 8.1 kwa mwaka ikilinganishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi kwa asilimia 6.3 mwezi Novemba 2024.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Kwa mwezi Septemba 2025, ukusanyaji wa mapato ya Serikali ukijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ulikuwa shilingi bilioni 3,718.2 sawa na ongezeko la asilimia 6.1 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, Serikali Kuu ilikusanya shilingi bilioni 3,570.4, na kiasi kilichobakia kilikusanywa na mamlaka za serikali za mitaa.

Makusanyo ya kodi ya mapato yalifikia shilingi bilioni 3,124.1 , sawa na ongezeko la asilimia 11.4 ya lengo. Mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato ni matokeo ya jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na usimamizi wa kodi (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Septemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

Serikali imeendelea kutekeleza bajeti yake kulingana na upatikanaji mapato. Jumla ya matumizi ya Serikali kwa mwezi Septemba 2025 yalikuwa shilingi bilioni 4,284.2, ambapo shilingi bilioni 2,508.6 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 1,775.6 zilielekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Septemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa (likijumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 51,870.3 mwishoni mwa mwezi Novemba 2025, sawa na ongezeko la asilimia 0.4 ikilinganishwa na deni lililofikiwa mwishoni mwa Oktoba 2025. Kati ya kiasi hicho, asilimia 69.7 ilikuwa ni deni la nje.

### Deni la nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 0.3 mwishoni mwa mwezi Novemba 2025 kutoka mwezi uliotangulia, na kufikia dola za Marekani milioni 36,127.8. Katika kiasi hicho, asilimia 80.5 ilikuwa deni la nje la Serikali, huku sehemu iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Mikopo iliyopokelewa kutoka nje ya nchi kwa mwezi Novemba 2025 ilikuwa dola za Marekani milioni 200.4, ambapo sehemu kubwa ilielekezwa Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 109.0 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 75.4 zilitumika kufanya malipo ya deni la msingi na kiasi cha dola za Marekani milioni 33.6 ni malipo ya riba.

Mchanganuo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji umeonesha kuwa, Mashirika ya Fedha ya Kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu kwa asilimia 56.5, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Aidha, mikopo iliyotumika kwa ajili ya urari wa malipo ya nje, na utekelezaji wa bajeti (BOP and budget support) iliongoza kwa asilimia 22.5 ikifuatiwa na mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66.8 ya deni, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Nov-24 Kiasi | Nov-24 Mchango (%) | Okt-25$^{r}$ Kiasi | Okt-25$^{r}$ Mchango (%) | Nov-25$^{p}$ Kiasi | Nov-25$^{p}$ Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,104.8 | 57.1 | 20,406.4 | 56.6 | 20,427.2 | 56.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,073.5 | 57.0 | 20,359.7 | 56.5 | 20,380.1 | 56.4 |
| Malimbikizo ya riba | 31.3 | 0.1 | 46.7 | 0.1 | 47.1 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,207.3 | 3.8 | 1,526.5 | 4.2 | 1,507.3 | 4.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,129.9 | 3.6 | 1,447.8 | 4.0 | 1,428.3 | 4.0 |
| Malimbikizo ya riba | 77.4 | 0.2 | 78.7 | 0.2 | 79.0 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,230.3 | 35.4 | 13,018.4 | 36.1 | 13,119.8 | 36.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,919.1 | 34.4 | 12,524.0 | 34.8 | 12,592.4 | 34.9 |
| Malimbikizo ya riba | 311.3 | 1.0 | 494.4 | 1.4 | 527.4 | 1.5 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,156.7 | 3.6 | 1,082.5 | 3.0 | 1,073.4 | 3.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 993.7 | 3.1 | 890.0 | 2.5 | 878.0 | 2.4 |
| Malimbikizo ya riba | 163.0 | 0.5 | 192.5 | 0.5 | 195.4 | 0.5 |
| Jumla ya deni la nje | 31,699.1 | 100.0 | 36,033.7 | 100.0 | 36,127.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Nov-24 Kiasi | Nov-24 Mchango (%) | Okt-25$^{r}$ Kiasi | Okt-25$^{r}$ Mchango (%) | Nov-25$^{p}$ Kiasi | Nov-25$^{p}$ Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,104.8 | 57.1 | 20,406.4 | 56.6 | 20,427.2 | 56.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,073.5 | 57.0 | 20,359.7 | 56.5 | 20,380.1 | 56.4 |
| Malimbikizo ya riba | 31.3 | 0.1 | 46.7 | 0.1 | 47.1 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,207.3 | 3.8 | 1,526.5 | 4.2 | 1,507.3 | 4.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,129.9 | 3.6 | 1,447.8 | 4.0 | 1,428.3 | 4.0 |
| Malimbikizo ya riba | 77.4 | 0.2 | 78.7 | 0.2 | 79.0 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,230.3 | 35.4 | 13,018.4 | 36.1 | 13,119.8 | 36.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,919.1 | 34.4 | 12,524.0 | 34.8 | 12,592.4 | 34.9 |
| Malimbikizo ya riba | 311.3 | 1.0 | 494.4 | 1.4 | 527.4 | 1.5 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,156.7 | 3.6 | 1,082.5 | 3.0 | 1,073.4 | 3.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 993.7 | 3.1 | 890.0 | 2.5 | 878.0 | 2.4 |
| Malimbikizo ya riba | 163.0 | 0.5 | 192.5 | 0.5 | 195.4 | 0.5 |
| Jumla ya deni la nje | 31,699.1 | 100.0 | 36,033.7 | 100.0 | 36,127.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

### Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Matumizi, kwa Asilimia

| Shughuli ya uchumi | Nov-24 | Okt-25$^{r}$ | Nov-25$^{p}$ |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 19.1 | 22.6 | 22.5 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.6 | 21.3 | 21.5 |
| Kilimo | 4.9 | 5.1 | 5.3 |
| Nishati na madini | 13.4 | 12.3 | 12.2 |
| Viwanda | 3.5 | 3.8 | 3.8 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.4 | 19.1 | 19.0 |
| Fedha na bima | 4.7 | 4.2 | 4.2 |
| Utalii | 1.6 | 1.7 | 1.7 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Mengineyo | 5.6 | 4.7 | 4.7 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali.

### Jendwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa Asilimia

| Sarafu | Nov-24 | Okt-25$^{r}$ | Nov-25$^{p}$ |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 67.1 | 66.7 | 66.8 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.6 | 17.3 | 17.3 |
| Yuan ya China | 6.3 | 6.3 | 6.3 |
| Sarafu nyinginezo | 10.0 | 9.6 | 9.6 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 38,361.3 mwishoni mwa mwezi Novemba 2025, sawa na ongezeko la asilimia 0.2 ikilinganishwa na mwezi uliotangulia (Kielelezo 2.6.1). Sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali imeendelea kuwa dhamana za muda mrefu, wakati benki za biashara, na mifuko ya hifadhi za jamii, zikiendelea kuwa wadai wakuu (Jedwali 2.6.5 na 2.6.6).

### Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

### Jedwali 2.6.5: Deni la Ndani la Serikali Kuu kwa Vyanzo vya Mikopo

Shilingi Bilioni

| | Nov-24 | | Okt-25$^{r}$ | | Nov-25$^{p}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 28,459.2 | 84.8 | 32,801.7 | 85.7 | 32,976.5 | 86.0 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,027.4 | 6.0 | 2,079.5 | 5.4 | 2,082.5 | 5.4 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 26,244.7 | 78.2 | 30,586.4 | 79.9 | 30,758.2 | 80.2 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,110.0 | 15.2 | 5,493.1 | 14.3 | 5,384.8 | 14.0 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,091.6 | 15.2 | 5,493.1 | 14.3 | 5,384.8 | 14.0 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 33,569.2 | 100.0 | 38,294.8 | 100.0 | 38,361.3 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine ya najumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

### Jedwali 2.6.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji

Shilingi Bilioni

| | Nov-24 | | Okt-25$^{r}$ | | Nov-25$^{p}$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,679.6 | 28.8 | 10,899.8 | 28.5 | 11,046.1 | 28.8 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 7,051.7 | 21.0 | 7,301.8 | 19.1 | 7,193.5 | 18.8 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,015.3 | 26.9 | 10,248.3 | 26.8 | 10,276.8 | 26.8 |
| Kampuni za bima | 1,921.8 | 5.7 | 2,020.0 | 5.3 | 2,008.8 | 5.2 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 460.4 | 1.4 | 749.5 | 2.0 | 749.8 | 2.0 |
| Wengine | 5,440.4 | 16.2 | 7,075.4 | 18.5 | 7,086.3 | 18.5 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 33,569.2 | 100.0 | 38,294.8 | 100.0 | 38,361.3 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na “wengine” inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Novemba 2025, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 442.7 kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana zake, kwa lengo la kufadhili nakisi ya bajeti (Kielelezo 2.6.2). Aidha, malipo ya deni la ndani yalikuwa shilingi bilioni 515.3,

yakijumuisha shilingi bilioni 267.9 kama malipo ya deni la msingi na shilingi bilioni 247.4 malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje imeendelea kuimarika katika mwaka unaoishia Novemba 2025, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida imepungua na kufikia dola za Marekani milioni 1,907.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,687.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Jedwali 2.7.1). Kuimarika huku kumechangiwa na ongezeko za mauzo ya nje ya bidhaa na huduma ikilinganishwa na uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi.

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa toshelevu, ikifikia dola za Marekani milioni 6,432.9 mwezi Novemba 2025. Kiwango hiki kinatosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.9 ambayo ni juu ya lengo la kitaifa na Jumuiya ya Afrika Mashariki la angalau miezi 4 (Chart 2.7.1).

**Jedwali 2.7.1 Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali**

Dola za Marekani Milioni

| | Nov-24 | | Okt-25r | | Nov-25P | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 28,459.2 | 84.8 | 32,801.7 | 85.7 | 32,976.5 | 86.0 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,027.4 | 6.0 | 2,079.5 | 5.4 | 2,082.5 | 5.4 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 26,244.7 | 78.2 | 30,586.4 | 79.9 | 30,758.2 | 80.2 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,110.0 | 15.2 | 5,493.1 | 14.3 | 5,384.8 | 14.0 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,091.6 | 15.2 | 5,493.1 | 14.3 | 5,384.8 | 14.0 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 33,569.2 | 100.0 | 38,294.8 | 100.0 | 38,361.3 | 100.0 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

### Mauzo ya Nje

Mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 13.1 na kufikia dola za Marekani milioni 17,561.5 kwa mwaka unaoishia Novemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 15,521.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, huduma za utalii, usafirishaji na bidhaa asilia, hususan tumbaku na korosho.

Mauzo ya bidhaa yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 10,172 katika mwaka unaoishia Novemba 2025, kutoka dola za Marekani milioni 8,760 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 . Ongezeko hili lilitokana zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku, korosho na kahawa(Kielelezo 2.7.2). Mathalani, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 42.1 hadi dola za Marekani milioni 4,719.8, kuliko changiwa na ongezeko la bei katika soko la dunia pamoja na uzalishaji nchini.

Mauzo ya bidhaa asilia yalifikia dola za Marekani milioni 1,391.7 sawa na asilimia 3.1. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na bei. Vilevile, mauzo ya nafaka yaliongezeka kwa asilimia 15.1 na kufikia dola za Marekani milioni 286.1, yakichangiwa zaidi na mauzo ya mahindi na mchele. Kwa mwezi Novemba 2025, mauzo ya bidhaa yalifikia dola za Marekani milioni 1,098.5 ikiwa ni zaidi ya dola za Marekani milioni 1,032.4 mwezi Novemba 2024, yakichangiwa zaidi na

mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani na tumbaku.

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Novemba 2025, mapato ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufikia dola za Marekani milioni 7,387.5, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,761.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mapato ya utalii na usafirishaji, ambapo, mapato ya utalii yalitokana na ongezeko la idadi ya watalii kutoka 2,106,870 mwaka unaoishia Novemba 2024 hadi 2,315,478 mwaka unaoishia Novemba 2025, sawa na ongezeko la asilimia 9.9. Mapato ya usafirishaji yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,772.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,325.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, yakichangiwa zaidi na gharama za usafirishaji wa bidhaa kwenda na kutoka nchi jirani (Kielelezo 2.7.3). Katika kipindi kinachoishia Novemba 2025, bidhaa zilizosafirishwa kupitia Tanzania (Transit goods) ziliongezeka kwa asilimia 37.3 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa mwezi Novemba 2025, mapato ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 593.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 589.7 mwezi Novemba 2024.

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

## Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje

Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 17,757.1 katika kipindi cha mwaka unaoishia Novemba 2025 kutoka dola za Marekani milioni 16,863.9 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Bidhaa za viwandani, mashine na mitambo, vifaa vya usafirishaji viwandani, na gharama za usafirishaji bidhaa zilizoagizwa ndio vilichangia zaidi ongezeko hili. Hata hivyo, katika kipindi husika, uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli, ulipungua kwa asilimia 7.1 na kufikia dola za Marekani milioni 2,396.4, sambamba na kupungua kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia. Kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa ulipungua hadi dola za Marekani milioni 1,257.4 Novemba 2025 kutoka dola za Marekani milioni 1,317 mwezi Novemba 2024.

**Kielelezo 2.7.4: Uagizaji wa Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi p inamaanisha takwimu za awali.

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Novemba 2025, malipo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 14.4 na kufikia dola za Marekani milioni 3,114.1 kutoka dola za Marekani milioni 2,722.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.7.5). Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na gharama za uagizaji bidhaa, sambamba na kuongezeka kwa uagizaji bidhaa nje ya nchi . Kwa mwezi Novemba 2025, malipo ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 270.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 267.7 mwezi Novemba 2024.

**Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo:Ukokotoaji wa Benki kuu ya Tanzania
